JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

AnwaniyaSimu:"UCHUNGUZI"
SimuNambari: 262323315
Nukushi: 26232332
BaruaPepe: dgeneral@pcc.go.tz
Tovuti: www.pccb.go.tz
Unapojibutafadhalitaja:

MtaawaJamhuri,

S. L. P 1291,
41101 DODOMA,
TANZANIA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

OKTOBA 16, 2019

MAAGIZO YA MHE RAIS YATEKELEZWA

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) inapenda kuufahamisha umma kwamba tayari imeanza kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais aliyoyatoa Jumanne Oktoba 15, 2019 wakati wa Mkutano wa Hadhara na Wananchi wa Wilaya ya Ruangwa Mjini, mkoani Lindi.

Kupitia hadhira hiyo, **Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliiagiza TAKUKURU pamoja na Mhe. Hussein Bashe, Naibu Waziri wa Kilimo kuhakikisha kuwa Vyama 10 vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) vinavyodaiwa na Wakulima vinawalipa wakulima husika kabla ya msimu wa Korosho kuanza vinginevyo wahusika wachukuliwe hatua kwa mujibu wa Sheria.

Utekelezaji wa Maagizo ya **Mhe. Rais** yameanza kutekelezwamara moja ambapo leo tarehe 16/10/2019 tayari TAKUKURU imefanikiwa kuwakamata Viongozi wa Vyama vya Msingi vya Ushirika(AMCOS) vifuatavyo;

(1) MILINDIMO AMCOS

Chama hiki kinadaiwa kiasi cha Tshs. 90, 711, 354.00 na wakulima wa ufuta fedha ambazo hazijalipwa mapaka hivi sasa. Viongozi waliokamatwa kutokana na kutolipa deni tajwa hapo juu ni;

i. Hemedi Yasin Kilete – Mwenyekiti
ii. Said hemedi Mkwera – Katibu
iii. Twahil Kilete – Karani
iv. Hillard Cosmas Chadili - Karani
v. Hassan Lidemu – Karani

Viongozi tajwa hapo juu wameshikiliwa na TAKUKURU Kwaajili ya uchunguzi pamoja na urejeshwaji wa fedha wanazodaiwa na Wakulima wa ufuta.

(2) MTUNAO AMCOS

Chama hiki kinadaiwa kiasi cha Tshs. 73, 715, 760.00 na wakulima wa ufuta fedha ambazo hazijalipwa mapaka hivi sasa. Viongozi waliokamatwa kutokana na kutolipa deni tajwa hapo juu ni;

vi. Hassan Ligunja – Katibu
vii. Karimu Ngara – Karani

Viongozi tajwa hapo juu wameshikiliwa na TAKUKURU Kwaajili ya uchunguzi pamoja na urejeshwaji wa fedha wanazodaiwa na Wakulima wa ufuta.

(3) KIPELELE AMCOS.

Chama hiki kinadaiwa kiasi cha Tshs. 57, 257, 280.00 na wakulima wa ufuta fedha ambazo hazijalipwa mapaka hivi sasa. Viongozi waliokamatwa kutokana na kutolipa deni tajwa hapo juu ni;

i. Zuberi Omary Nolele – Mwenyekiti
ii. Mjamari Haji Kibohu – Katibu

Viongozi tajwa hapo juu wameshikiliwa na TAKUKURU Kwaajili ya uchunguzi pamoja na urejeshwaji wa fedha wanazodaiwa na Wakulima wa ufuta.

(4) NACHIUNGA AMCOS

Chama hiki kinadaiwa kiasi cha Tshs. 10, 780, 100.00 na wakulima wa ufuta fedha ambazo hazijalipwa mapaka hivi sasa. Viongozi waliokamatwa kutokana na kutolipa deni tajwa hapo juu ni;

i. Said Mohamed Mbunda – Makamu Mwenyekiti
ii. Mathiad Mohamed Likumwili – Mjumbe
iii. Chande Mshamu Mandadu – Mjumbe
iv. Issa Lutumno – Mjumbe
v. Nasra Chigwile - Karani

(5) CHIKONJI AMCOS.

Chama hiki kinadaiwa kiasi cha Tshs. 10, 325, 550.00 na wakulima wa ufuta fedha ambazo hazijalipwa mapaka hivi sasa. Viongozi waliokamatwa kutokana na kutolipa deni tajwa hapo juu ni;

i. Abdallah Athumani Mtala – Mwenyekiti
ii. Karimu Bakari Maguto – Katibu
iii. Hussein Said Huessein – Mjumbe
iv. Latifa Abdallah – Karani
v. Amina Issa Mtauna - Mjumbe

Viongozi tajwa hapo juu wameshikiliwa na TAKUKURU Kwaajili ya uchunguzi pamoja na urejeshwaji wa fedha wanazodaiwa na Wakulima wa ufuta.

(6) KINJEKITILE AMCOS

Chama cha hiki kinadaiwa kiasi cha Tshs. 15,100,000/- wakulima wa ufuta fedha ambazo zilikuwa deni la ufuta. Kiongozi aliyekamatwa kutokana na deni tajwa hapo juu ni;

i. Hussen Ally Mnindi – Katibu,

Baada ya viongozi tajwa hapo juu kukamatwa na kuhojiwa na TAKUKURU wamewasilisha TAKUKURU fedha yote wanayodaiwa na wakulima wa ufuta ili wakulima hao walipwe fedha zao.

(7) MTAMA AMCOS

Chama hiki kinadaiwa kiasi cha Sh. 8,523,830.00na wakulima wa ufuta pamoja na Sh. 160,000.00 na Chama Kikuu cha Ushirika (ILULU AMCOS) fedha ambazo zilikuwa deni la ufuta. Viongozi waliokamatwa kutokana na deni tajwa hapo juu ni;

i. Zainabu Khalfa – MAKAMU Mwenyekiti,
ii. Bashiri Ally – Katibu,
iii. Abdallah Abdallah – Katibu Msaidizi
iv. Haji Juma Namangaya – Karani
v. Mohamed Abrahaman Ligoli – Karani
vi. Saidi Hashi Nguri – Karani
vii. Pius Lucas – Karani
viii. Abrahaman Mohamed Kapanda – Karani

Baada ya viongozi tajwa hapo juu kukamatwa na kuhojiwa na TAKUKURU wamekamilisha kulipa deni wanalodaiwa na wakulima wa ufuta pamoja na na Chama Kikuu cha Ushirika (ILULU AMCOS).

(8) MATUMBI AMCOS

Chama hiki kinadaiwa kiasi cha Sh. 12,154,604/- wakulima wa ufuta fedha ambazo zilikuwa deni la ufuta. Viongozi waliokamatwa kutokana na deni tajwa hapo juu ni;

i. Ally Kinyemela Mtombo – Katibu,
ii. Mshamu Mohamed Ngurangwa - Karani

Baada ya viongozi tajwa hapo juu kukamatwa na kuhojiwa na TAKUKURU wamewasilisha TAKUKURU kiasi cha Sh. 5,937,000.00 na kiasi kilichobakia cha Sh. 6,217,604.00 kitalipwa tarehe 30/10/2019.

(9) RUANGWA – MANDAWA AMCOS.

Chama hiki kinadaiwa kiasi cha Sh. 4,095,200.00 wakulima wa ufuta fedha ambazo zilikuwa deni la ufuta. Viongozi waliokamatwa kutokana na deni tajwa hapo juu ni;

i. Nurdin Hashhim Ndope – Mwenyekiti,
ii. Shaibu Omary Matumbi - Katibu
iii. Hamza M Kumtitima – katibu Masaidizi,
iv. Mustafa Juma Chiumbo – Mjumbe,
v. Seleman M. Mtonda – Mjumbe
vi. Mpanjila Bakari Mpanjila - Karani

Baada ya viongozi tajwa hapo juu kukamatwa na kuhojiwa na TAKUKURU wamewasilisha TAKUKURU fedha yote wanayodaiwa na wakulima wa ufuta ili wakulima hao walipwe fedha zao.

(10) MCHINGA AMCOS

Chama hiki kinadaiwa kiasi cha Sh. 3,604,500/- wakulima wa ufuta fedha ambazo zilikuwa deni la ufuta. Viongozi waliokamatwa kutokana na deni tajwa hapo juu ni;

ii. Mussa Selemani Maringa – Mwenyekiti,
iii. Japhari Said Likwena – Makamu Mwenyekiti,

iv. Patrick Magnus Martine - katibu,
v. Abdalah Selemani Maringa – Mjumbe wa Bodi,
vi. Hassan Masoud Mteremko – karani

Baada ya viongozi tajwa hapo juu kukamatwa na kuhojiwa na TAKUKURU wamewasilisha TAKUKURU fedha yote wanayodaiwa na wakulima wa ufuta ili wakulima hao walipwe fedha zao.

(11) MNOLELA AMCOS.

Chama hiki kinadaiwa kiasi cha Sh. 3,052,000.00 na wakulima wa ufuta fedha ambazo zilikuwa deni la ufuta. Viongozi waliokamatwa kutokana na deni tajwa hapo juu ni;

i. Salim Ismail Mkopi – Mwenyekiti
ii. Hamida Hamisi Kaulu – Makamu Mwenyekiti
iii. Masoud Hamisi – Katibu
iv. Nadhifu Nauka – Katibu Msaidizi
v. Ismail Hamisi Namjupa – Mjumbe wa Bodi

Baada ya viongozi tajwa hapo juu kukamatwa na kuhojiwa na TAKUKURU wamekamilisha kulipa deni wanalodaiwa na wakulima wa ufuta.

(12) MMANGAWANGA AMCOS

Chama hiki kinadaiwa kiasi cha Sh. 3,314,300.00 na wakulima wa ufuta fedha ambazo zilikuwa deni la ufuta. Viongozi waliokamatwa kutokana na deni tajwa hapo juu ni;

i. Said I. Mchia – Mwenyekiti

ii. Aziz H. Machemba – Katibu
iii. Abubakari R. Maharage – Mjumbe

Baada ya viongozi tajwa hapo juu kukamatwa na kuhojiwa na TAKUKURU wamekamilisha kulipa deni wanalodaiwa na wakulima wa ufuta.

(13) MAGEUZI AMCOS.

Chama hiki kinadaiwa kiasi cha Sh. 2,630,000.00 na wakulima wa ufuta fedha ambazo zilikuwa deni la ufuta. Viongozi waliokamatwa kutokana na deni tajwa hapo juu ni;

i. Sudi Nyarubi Mpili – Mwekiti
ii. Saidi Ally Likotea – katibu
iii. Bakari nyarubi Mpili – mjumbe

Baada ya viongozi tajwa hapo juu kukamatwa na kuhojiwa na TAKUKURU wamekamilisha kulipa deni wanalodaiwa na wakulima wa ufuta.

Viongozi tajwa hapo juu wameshikiliwa na TAKUKURU Kwaajili ya uchunguzi pamoja na urejeshwaji wa fedha wanazodaiwa na Wakulima wa ufuta.

Tangu TAKUKURU imeanza zoezi la kuhakikisha AMCOS zinazodaiwa na wakulima wa Ufuta zinarejesha fedha zinazodaiwa, imefanikiwa kurejesha kiasi cha Sh. 46,416,830.00.

Ninapenda Wananchi wajue kuwa zoezi hili ni endelevu na halitokoma mpaka tuhakikishe wakulima wote wamelipwa stahili zao kwa mujibu wa Sheria.

Zoezi hili linaendelea kwa kufuatilia madeni ya wakulima katika AMCOS zifuatazo:-

(i) Nyangamara AMCOS inadaiwa Tshs.45,364,610.00
(ii) Namangale AMCOS inadaiwa Tshs.8,97,650.00
(iii) Nahukahuka AMCOS inadaiwa Tshs.6,160,500.00
(iv) Mtua AMCOS inadaiwa Tshs.1,628,100.00
(v) Kingoli AMCOS inadaiwa Tshs.4,032,593.00
(vi) Malungo AMCOS inadaiwa Tshs.1,864,670.00
(vii) Mandwanga AMCOS inadiwa Tshs.3,542,400.00
(viii) Nanjilinji "A"AMCOS inadiwa Tshs.49,334,400.00
(ix) Zinga AMCOSinadiwa Tshs.117,435,685.00
(x) Rutamba AMCOS inadiwa Tshs.6,378,130.00
(xi) Nyangamara AMCOS inadiwa Tshs.45,364,610.00
(xii) Naambu AMCOS inadiwa Tshs31,409,610.00
(xiii) Mbemkuru AMCOSinadiwa Tshs 35,803,804.00
(xiv) Mlindimo AMCOM inadiwa Tshs 85,271,743.00
(xv) Mtunaho AMCOS inadiwa Tshs 50,678,460.00

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) inatoa rai kwa jamii ya wakulima na wafanyabiashara wa korosho kuwa haina utani katika utekezaji wa maelekezo haya.

Ni rai yangu kuwa Viongozi wote wa Vyama vya Ushirika vinavyodaiwa na Wakulima viwalipe wakulima hao HARAKA IWEZEKANAVYO kabla TAKUKURU haijawafikia. Ninataka wahusika wafahamu kwamba katika zoezi hili hakuna chama cha ushirika kinachodaiwa ambacho kitabaki salama.

Zoezi la ufuatliaji wa malipo ya Wakulima kwa Vyama vya Ushirika ni Endelevu na pindi litakapokamilika tutatoa taarifa kamili.

UBADHILIFU WA FEDHA KIASI CHA SH. 221,00,000.00 KATIKA HOSPITALI YA MKOA (HOSPITALI YA SOKOINE)

Pia leo tarehe 16/10/2019 TAKUKURU (M) LINDI INAWASHIKILIA Ndg. GEORGE CLEMENCE OLOMI Mhasibu wa Hospitali ya Mkoa wa LINDI na Ndg. ZEBEDAYO SELEMANI ambaye ni Mhandisi Msaidizi wa Halmashauri (W) LINDI kwa makosa ya Ubadhilifu wa fedha za Mradi wa Ujenzi wa Wodi ya watoto na choo cha wagonjwa na maabara.

Watuhumiwa hao wanatuhumiwa kuandaa nyaraka za malipo hewa na kufanya malipo yanayozidi kiwango kilichoainishwa kwenye Mikataba iliyoingiwa na Wazabuni mbalimbali.

Uchunguzi wa tuhuma hii bado unaendelea na pindi utakapokamilika tutatoa taarifa.

WITO:

Tunaendelea kuwasihi wananchi wenye ushahidi wa mambo haya ambao ama wamedhulumiwa au kuhujumiwa kwa namna yoyote ile katika biashara hii ya Ufuta, wasisite kutupatia taarifa ili nasi tuchukue hatua stahiki mara moja. Ni lazima tukumbuke kwamba msingi wa maendeleo ya wananchi wa mkoa huu yatategemea sana ustawi na uimara wa Vyama vya Ushirika, hivyo kila mmoja wenu awe mstari wa mbele katika kuwafichuwa wale wote wenye nia ovu ya kuihujumu biashara hii ikiwa ni pamoja na kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Ninawasihi tuendelee kumuunga mkono Rais wetu **Mhe. Dkt John Pombe Joseph Magufuli** ambaye siku zote amekuwa mstari wa mbele katika kuongoza mapambano dhidi ya rushwa. Vilevile tunawasihi wananchi kuwa tayari kutoa ushahidi katika chunguzi mbalimbali zinazochunguzwa na TAKUKURU ili kuunga mkono jitihada za mapambano dhidi ya rushwa nchini.

IMETOLEWA NA:

BRIG.JEN. JOHN J. MBUNGO
KAIMU MKURUGENZI MKUU
TAKUKURU